**KIZIDUO**

**MUHTASARI WA KIKAO CHA TIMU YA MENEJIMENTI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA KILICHOFANYIKA TAREHE 11.10.2021 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA OFISI YA HALMASHAURI YA KIJIJI CHA KITANGARI SOKONI.**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA.**

1. Ndg. Magreth Likonda - Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) - Mwenyekiti
2. Ndg. Bahati E. Mazengo. - Kaimu Afisa Utumishi (W) - Katibu
3. Ndg. Lucy I. Matem - Afisa Sheria
4. Ndg. Sijali B. Mabena - Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
5. Ndg. Ally Mlaponi - Kaimu Mweka Hazina (W)
6. Ndg. Elias A. Mwalusamba - Afisa Ugavi (W)
7. Ndg. Shada Nankoko - Kaimu Afisa Elimu Msingi (W)
8. Ndg. Allan P.Daniel - Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W)
9. Ndg. Alford Mpanda - Afisa Elimu Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W)
10. Ndg. Denis Kaguo - Kaimu Mkaguzi wa Ndani (W)
11. Ndg. Hamisi Mahamoud - Afisa Tehama
12. Ndg. Geofrey Chitanda - Afisa Maendeleo ya Jamii (W)
13. Ndg. Christina Malombe - Kaimu Mganga Mkuu (W)
14. Ndg. Ponsiana J. Moyo - Mwandishi wa Vikao
15. Ndg. Nguche Nankutwa - Kaimu Afisa Mipango (W)
16. Ndg. Anna P. Nade - Afisa Ardhi
17. Ndg. Tumain Y. Sadick - Afisa Usimamizi wa Mazingira.
18. Ndg. Rashid Mabaya - Mwandishi wa Vikao
19. Ndg. Hamis Kundindo - Mwandishi wa vikao

**MUHTASARI NA 17/2021/2022: KUFUNGUA KIKAO.**
Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe katika Kikao cha Timu ya Menejimenti na aliwaomba kujadili kwa kina agenda zote zitakazowasilishwa. Alifungua kikao saa 04:23 mchana.

**MUHTASARI NA 22/2021/2022: TAARIFA YA MAPOKEZI NA MATUMIZI YA FEDHA ZA UVIKO-19 NJE YA BAJETI TSHS. 1,170,000,000.00 KWA MWAKA 2021/2022.**

Kaimu Afisa Mipango (W) aliwasilisha taarifa ya mapokezi na matumizi ya fedha za Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya Uviko-19 kiasi cha *Tshs. 1,170,000.000.00* fedha ambazo ambazo zitatekeleza miradi ya Sekta za Elimu Msingi *Tshs.240,000,000.00* Elimu Sekondari *Tshs. 540,000,000.00* na Afya *Tshs. 390,000,000.00* Pia alisema kuwa maelezo ya jumla ya utekelezaji wa wa fedha hizi ni pamoja na Halmashauri zinaweza kutumia Wakandarasi wa ndani au utaratibu wa "*Force Account*", gharama za utekelezaji kwa kutumia njia yeyote zisizidi makadirio ya fedha zilizotengwa kwa shughuli husika,



CS CamScanner

kuhakikisha miradi inakamilika ifikapo tarehe 15.12.2021 na miradi mingine ifikapo tarehe 30.04.2022, aidha miradi ioneshe thamani ya fedha na ubora wa miradi.

### i. SEKTA YA ELIMU MSINGI - UJENZI WA MIUNDOMBINU SHULE SHIKIZI

| S/N | SHULE NA MIUNDOMBINU | MAKISIO YA FEDHA |
|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa madarasa 2- Shule ya Msingi Mdimba | 40,000,000.00 |
| 2. | Ujenzi wa madarasa 2- Shule ya Msingi Mpalu | 40,000,000.00 |
| 3. | Ujenzi wa madarasa 2- Shule ya Msingi Nakahako | 40,000,000.00 |
| 4. | Ujenzi wa madarasa 2- Shule ya Msingi Vihokoli | 40,000,000.00 |
| 5. | Ujenzi wa madarasa 2- Shule ya Msingi Mnolela | 40,000,000.00 |
| 6. | Ujenzi wa madarasa 2- Shule ya Msingi Namdimba | 40,000,000.00 |
| | **JUMLA** | **240,000,000.00** |

### ii. SEKTA YA ELIMU SEKONDARI

| S/N | SHULE NA MIUNDOMBINU | MAKISIO YA FEDHA |
|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa madarasa 2 – Shule ya Sekondari Mikumbi | 40,000,000.00 |
| | Ujenzi wa madarasa 2 – Shule ya Sekondari Chitekete | 40,000,000.00 |
| | Ujenzi wa madarasa 3 – Shule ya Sekondari Mpotola | 60,000,000.00 |
| | Ujenzi wa madarasa 2 – Shule ya Sekondari Makukwe | 40,000,000.00 |
| | Ujenzi wa madarasa 2 – Shule ya Sekondari Maputi | 40,000,000.00 |
| | Ujenzi wa madarasa 2 – Shule ya Sekondari Lengo | 40,000,000.00 |
| | Ujenzi wa madarasa 2 – Shule ya Sekondari Ushirika | 40,000,000.00 |
| | Ujenzi wa madarasa 4 – Shule ya Sekondari Mnyambe | 80,000,000.00 |
| | Ujenzi wa madarasa 4 – Shule ya Sekondari Mtopwa | 80,000,000.00 |
| | Ujenzi wa madarasa 2 – Shule ya Sekondari Mkoma | 40,000,000.00 |
| | Ujenzi wa madarasa 2 – Shule ya Sekondari Vihokoli | 40,000,000.00 |
| | **JUMLA** | **540,000,000.00** |

### iii. SEKTA YA AFYA

| S/N | KITUO NA MIUNDOMBINU | MAKISIO YA FEDHA |
|---|---|---|
| | Ujenzi wa Jengo la dharura – Hospitali ya Wilaya | 300,000,000.00 |
| | Ujenzi wa nyumba ya Mtumishi wa Afya ya kaya 3 | 90,000,000.00 |
| | **JUMLA** | **390,000,000.00** |
| | **JUMLA KUU YA MGAO WA FEDHA ZA UVIKO-19** | **1,170,000,000.00** |

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo:

Wajumbe walishauri kuwa ni vyema wakati wa utekelezaji wa miradi hii maelekezo yaliyotolewa yakazingatiwa ili kuhakikisha miradi hii inaonesha thamani ya fedha na ubora unaofaa.



CamScanner

Mjumbe alishauri kuwa ni vyema jamii inakahamishwa katika utekelezaji wa miradi hii kwasababu moja ya njia ya utekelezaji wake ni njia ya Force Account ili kuipa jamii utambuzi na ushiriki wa kina katika utekelezaji wa miradi hii.

Kaimu Afisa Mipango (W) alipokea ushauri uliotolewa na wajumbe na kusema kuwa yote yakizingatiwa kwa ushirikiano wa Menejimenti, Wahe. Madiwani na Wanachi basi miradi hii itekelezwa kwa ufanisi.

Baada ya majadiliano Menejimenti ilipokea na kuridhia taarifa ya mapokezi na matumizi ya fedha za Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya Uviko-19 kiasi cha *Tshs. 1,170,000.000.00* kwa utekelezaji.

**MUHTASARI NA. 25/2021/2022- KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa mahudhurio yao katika kikao na alisisitiza kuwa yale ambayo wamejadili yafanyiwe kazi kwa utekelezaji. Alifunga kikao saa 07:12 mchana.

"UMETHIBITISHWANA"

KATIBU
JINA...RUKIA MOHAMED...
SAINI...............

MWENYEKITI
JINA...MABEKETI LILCOMNA...
SAINI...............

TAREHE...15.../...10.../2021.